

JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS –TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA ULANGA



Tarehe: 18/05/2020

TANGAZO LA ZABUNI  
NAMBA YA ZABUNI LGA/082/2020-2021/HQ/NC/01 Lot 1 – 4/ 04  
ZABUNI YA UKUSANYAJI USHURU MBALIMBALI WA VYANZO VYA MAPATO NA UZOAJI  
TAKA NGUMU KWA MWAKA 2020/2021

Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga inakusudia kuweka wazabuni wa Utozaji Ushuru wa vyanzo mbalimbali vya mapato kwa mwaka 2020/2021.

Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga inapenda kuwaalika watu Binafsi, Makampuni, Ushirika, Taasisi au Vikundi vya watu vilivyosajiliwa kisheria, wenye nia na uwezo wa kufanya kazi hizo, watume maombi yao kwa zabuni zifuatazo:-

NA.	AINA YA ZABUNI	NAMBA YA ZABUNI	ENEO LA KUKUSANYA USHURU
1.	Ushuru wa mazao ya chakula na nafaka	LGA/082/2020/2021/HQ/NC/01 - Lot 01	Eneo lote la Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga
2.	Ushuru wa Mazao ya Misitu i.e. Mbao, Mkaa, Nguzo, Mirunda, Magogo, Kuni na Mazao mengine ya misitu.	LGA/082/2020/2021/HQ/NC/01 - Lot 02	Eneo lote la Halmashauri ya Ulanga isipokuwa mazao ya kiwanda cha KVTC
3.	Ushuru wa Minada	LGA/082/2020/2021/HQ/NC/01 - Lot 03	Mnada wa Lukande, Iputi, Mavimba, Mbuyuni na Mbenja katika Halmshauri ya Wilaya ya Ulanga
4.	Ukusanyaji wa ushuru wa madini ya ujenzi i.e Mchanga, mawe, kokoto na kifusi.	LGA/082/2020/2021/HQ/NC/01 - Lot 04	Eneo lote la Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga
5.	Ukusanyaji ushuru wa taka, ukusanyaji wa taka ngumu na ubebaji kutoka Kata ya Mahenge mjini hadi Dampo la Mbagula	LGA/082/2020/2021/HQ/NC/04	Kata ya Mahenge Mjini

